

SWAHILI FORUM 12 (2005): 109-120

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

YARED M. KIHORE

1. Utangulizi

Sarufi inafafanuliwa kama kanuni, sheria au taratibu zinazotawala katika viwango vyote vya uchambuzi wa lugha ambavyo ni umbosauti (au fonolojia), umboneno (au mofolojia), miundomaneno (au sintaksia) na umbomaana (au semantiki). Kila lugha ina kanuni au sheria zake zinazotawala katika kila kiwango kilichotajwa.

Kwa wasemaji wa kawaida wa lugha, kanuni hizi hujidhihirisha hasa kuhusiana na mpangilio wa sauti kuunda maneno na wa maneno kuunda sentensi na misemo mingine mbalimbali. Kwa mfano, katika Kiswahili kanuni zinazotawala katika kiwango cha umbosauti katika lugha hiyo ni zile:

- (a) zinazoonyesha orodha ya vitamkwa vinavyotumika katika lugha hiyo (yaani konsonanti ngapi na zipi, irabu ngapi na zipi).
- (b) za sifa za mahali na jinsi ya kutamka vitamkwa hivyo (kama vile midomo, meno, kipasuo, kimadende).
- (c) za mpangilio wa vitamkwa hivyo kuunda maumbo yanayokubalika katika lugha hiyo (kwa mfano dodo, ng'ombe).

Lugha hii, mathalani, huruhusu zaidi konsonanti kufuatwa na irabu hasa katika utaratibu wake wa kawaida wa uundaji wa silabi zake kama katika so/ma = soma, la/la = lala, ku/la = kula, na ka-dhalika. Kwa mujibu wa Massamba, Kihore & Msanjila (2004: 10), silabi ni “kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi ambacho kwacho sauti za lugha hutamkwa kwa mara moja kama fungu moja”. Aidha katika lugha hii nazali peke yake inapotangulia konsonanti au inapoungana na konsonanti pia huweza kuwa silabi kama katika m/pa/ngo = mpango, n/ta = nta, m/ku/njo = mkunjo, ndo/a/na = ndoana. Zaidi ya hayo irabu nazo zinaweza zikafuatana katika umbo la neno na kila moja kuwa silabi kama katika o/a, u/a, a/u/a.

Lugha hii, kwa kawaida, hairuhusu miandamano ya konsonanti tofauti na hiyo iliyotajwa. Kwa mfano, hairuhusu miandamano ya konsonanti kama vile db, gb, kn, kt, na kahalika. Kiswahili pia, tofauti na baadhi ya lugha nyingine za Kibantu, huwa ina kanuni za wazi za kutokea kwa sauti [l] na [r] katika maumbo ya maneno kama katika kalamu/karamu, lika/rika, lia/ria, linda/rinda. Inaonekana mkanganyiko katika matumizi ya sauti hizi ambao bado yanajidhihirisha kwa wazi sana katika maandishi kwenye vyombo vya habari na katika usemaji wa baadhi ya watumia lugha nchini Tanzania ni matokeo ya athari ya lugha za kwanza za waandishi na watumiaji hao wa lugha.

Kanuni kama hizo zilizoelezwa kuhusiana na kiwango hicho cha umbosauti hujitokeza pia katika viwango vingine vilivyotajwa yaani vile vya umboneno, miundomaneno na umbomaana. Kuhusiana na masuala ya tafsiri, kanuni muhimu sana zinazopaswa kuzingatiwa ni zile za

kiwango cha miundomaneno au sentensi. Kanuni katika kiwango cha miundomaneno, kwa jumla, huwa zinahusu uchaguzi wa maneno sahihi katika muktadha wa maelezo na jinsi maneno kama hayo yanavyopangiliwa kuunda vipashio mbalimbali vya sentensi na sentensi zenye.

Uchaguzi wa maneno huweza kujidhihirisha kama ifuatavyo. Kwa mfano, unapotaka kuzungumzia dhana ya “kufanya tendo lisiendelee kufanyika” katika Kiswahili, huwa una orodha ya maneno kadhaa yanayoeleza dhana hiyo kwa namna mbalimbali. Katika lugha hii maneno yanayohusika na dhana hiyo ni kama vile *maliza, komesha, acha, simamisha, sitisha, katiza, katisha*. Maneno haya, japokuwa yote yanaeleza dhana kuu ya kufanya tendo lisiendelee kufanyika, kila moja lina muktadha wa matumizi linapotoa maana muafaka hasa. Hebu tuone jinsi maneno haya yanavyoweza kutumika kutafsiri sentensi mbalimbali za Kiingereza zenye neno ‘stop’:

- (1) (a) *He stopped the car.* = Alisimamisha gari.
- (b) *He stopped the programme before time.* = Alikatiza kipindi kabla ya muda.
- (c) *He stopped talking.* = Aliacha kuzungumza.
- (d) *He stopped the fight.* = Alisitisha mapigano/mapambano.

Hapa katika (1) tunaona jinsi sentensi mbalimbali za lugha ya Kiingereza zenye neno ‘stop’ zinavyotafsiriwa kwa maneno tofauti ya Kiswahili yenye dhana ya kufanya tendo lisiendelee kufanyika. Ukiyachunguza vizuri maneno haya ya Kiswahili, utaona kwamba kila moja linatoa maana muafaka pale lilipo; na likihamishwa kwenda katika sentensi nyingine hufanya sentensi hiyo isiweze kukubalika vizuri. Hii inaonyesha jinsi kulivyo na haja ya kuchagua neno sahihi hata pale unapotafsiri dhana moja kuu. Kwani, kwa kawaida, maana katika sentensi huwa inategemea neno linalobeba dhana kuu lilivyopangana na kufungamana na maneno mengine katika sentensi. Hivyo uchaguzi wa maneno yanayosadifu muktadha wa maelezo ni hatua ya kwanza muhimu ya kisarufi (yaani ya umboneno) inayohitaji kuzingatiwa.

Mifano katika (1) pia inadhihirisha jinsi mpangilio wa maneno katika sentensi nzima unavyofanya sentensi hiyo ieleweke. Inaonekana kwamba japokuwa sentensi zote katika (1) zinaeleza dhana moja kuu iliyobebwa na kitenzi kilekile katika lugha ya Kiingereza, maneno mbalimbali yanayojitokeza na kitenzi hicho hufanya kila sentensi kueleweka kwa namna yake na hivyo kuhitaji kutafsirika kwa namna tofauti. Hivyo, mpangilio wa maneno katika sentensi ni hatua ya pili ya kisarufi (yaani ya kimiundomaneno) ambayo nayo inapaswa kuzingatiwa katika tafsiri.

Hatua ya tatu ya kisarufi inayohitaji kuzingatiwa katika tafsiri pia ni ile ya umbomaana za miundo maalumu katika lugha kama vile methali, nahau na misemo mbalimbali. Hapa maana ndiyo huzingatiwa zaidi kuliko maneno yanayohusika katika tungo au jinsi yalivyopangiliwa. Hii ni kwa sababu katika kundi hili sifa yake moja muhimu ni kwamba, kwa kawaida, tungo zinazohusika zina maana ambazo huwa hazina uhusiano wa moja kwa moja na maana ya maneno yaliyotumika kuziunda. Kwa mfano, maana ya nahau “mkono mrefu”, haihusiani

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

moja kwa moja na maana za maneno yanayounda nahau hiyo. Hivyo, kutafsiri nahau hiyo kwa lugha ya Kiingereza kama “*long hand*” hakuleti maana ile iliyopo katika Kiswahili, lugha ilimoibukia nahau hiyo. Katika Kiswahili nahau hii ina maana ya mdokozi au mwizi

Kanuni au sheria zinazohusiana na masuala ya kisarufi yaliyotajwa, yaani, uchaguzi wa neno linalosadifu muktadha wa maelezo, maana inayotokana na mpangilio wa maneno katika sentensi nzima na maana za miundo maalumu kama methali, nahau, na nyinginezo, ndiyo tutakayoyajadili kwa undani katika makala haya.

Lakini kabla ya kuanza kujadili masuala hayo ya kisarufi yanayopaswa kuzingatiwa katika tafsiri, pengine ni muhimu pia katika utangulizi huu kuitazama kwa ufupi dhana ya ‘tafsiri’. Tafsiri hufafanuliwa kama jaribio la kuwasilisha ujumbe uleule ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine. Tafsiri hujihusisha hasa na maana na muundo wa lugha katika matini asilia na pia katika tafsiri yenyewe. Hii ina maana inajihusisha na viwango vya lugha tulivyoviita umbomaana na miundomaneno katika aya ya kwanza hapo juu.

Kwa jumla, huwa kuna aina mbili za tafsiri: (a) tafsiri halisi/sisisi (= *literal*) inayozingatia neno hata neno au hasa mpangilio wa maneno hayo katika sentensi za lugha katika matini asilia au chanzi; na (b) tafsiri huru (= *liberal*) inayozingatia zaidi maana iliyomo katika matini chanzi. Katika aina hizi za tafsiri, ile ya kwanza hukabiliwa na matatizo makubwa pale kunapokuwa na tofauti kubwa za kimuundo baina ya lugha chanzi na lugha ya tafsiri. Katika hali kama hiyo, ukitafsiri neno kwa neno utapata muundo katika tafsiri usiokuwa na maana yoyote. Ama kuhusu aina ya pili ya tafsiri, matatizo huwa ni uwezekano wa mfasiri kuongeza au kupunguza maana ya kinachotafsiriwa kupita kiasi (tz. kwa mfano Mugambi 2001: 225; Ohly 1976: 82-84). Kwa jumla, Nasution 1988 hufikiri kwamba aina hizi mbili za tafsiri hukiinzana.

2. Tafsiri na uzingatifu wa maneno muafaka

Kama tulivyoonyesha katika (1) hapo juu, hata neno moja peke yake likiwa katika mazingira ya sentensi tofauti za lugha moja linaweza likahitaji kutafsiriwa kwa maneno mbalimbali tofauti katika lugha nyingine. Hii ni kwa kuwa dhana moja kuu linalowakilishwa na neno moja katika lugha moja linaweza kuwakilishwa kwa maneno kadhaa katika lugha nyingine kila moja likisadifu mazingira fulani tu ya maelezo yanayotafsiriwa. Mifano zaidi ni hii ya sentensi za Kiingereza zenye neno as. Katika tafsiri kwa Kiswahili neno hili linawakilishwa na maneno tofauti katika Kiswahili kama inavyoonekana katika (2) hapa chini:

- (2) (a) “*But as Mbokola has observed...*” = Lakini kama Mbokola alivyohoji...
- (b) “*As African societies evolved into distinct ethnic groups...*” = Jamii za Kiafrika zilipofunuka katika mbari tofauti...
- (c) *He ran away as he couldn't stand the fight* = Alikimbia kwa kuwa hakuweza kustahimili mapigano

Mifano katika (2) inaonyesha neno ‘*as*’ katika sentensi hizo za Kiingereza likijitokeza kama kipengele ‘linganifu’ katika (2a), kipengele ‘sababishi’ katika (2b), na kipengele ‘cha kidunia’ katika (2c), na tafsiri yake inavyofanywa kwa maneno au maelezo tofauti kwa Kiswahili. Hali

hii inachangiwa, kwa kiasi, na nafasi ya neno hilo katika muundo na, kwa kiasi, na maana ya maelezo katika muundo. Hii ina maana kwamba tafsiri isitegemee tu maana moja ya neno anayojua mfasiri kwani hali hubadilika kulingana muundo wa sentensi neno hilo linapojitokeza.

Hali hiyo tunayoiona katika (2) inajitokeza pia katika Kiswahili pale neno moja linapokuwa na maana kadhaa, kila maana ikidhihirika tu katika muktadha wa sentensi ilimotumika. Kwa mfano, neno ‘-chukulia’ katika miktadha ya sentensi zifuatazo lina maana tofauti kabisa:

(3) (a) Alimchukulia Juma mzigo wake (= *She/he carried/took Juma's baggage for him*)

(b) Alichukulia kwamba mambo yatakwenda anavyotaka yeye (= *She/he assumed that things will go as she/he wants them to*)

Mifano katika (3) inaonyesha kwamba maana ya neno ‘-chukulia’ katika (3a) si sawa na maana yake katika (3b). Hapa, tofauti na hali tuliyoiona katika (2), neno ‘chukulia’ liko katika nafasi ileile ya mwanzoni mwa sentensi. Hivyo, kazi yoyote ya tafsiri ni muhimu izingatie matumizi haya ya kisarufi ya neno katika sentensi mbalimbali.

Suala la nafasi ya neno linapata umuhimu pia kuhusiana na miundo ya sentensi kama hizi katika (4):

(4) (a) Simba amemuua mtu (= *A lion has killed a person*)

(b) Mtu amemuua simba (= *A person has killed a lion*)

Sentensi katika (4), japokuwa zina maneno yaleyale, bado zinatofautiana kimaana, msingi mkubwa ukiwa ni maneno ‘simba’ na ‘mtu’ kubadilishana nafasi. Hii ina maana kwamba hata katika tafsiri umuhimu wa nafasi inayoshikwa na kila neno unapaswa kuzingatiwa.

Tunaona umuhimu wa kusisitiza katika sehemu hii kwamba kila lugha ina makundi mengi ya maneno yanayoeleza vivuli vya maana kuu fulani na si kila moja ya maneno kama hayo linaweza likapata kisawe chake katika lugha nyingine. Hii ni kwa sababu makundi hayo pia huwa yamekitwa katika misingi ya tamaduni za lugha hizo. Dhana ya mazingira ya kiutamaduni ya lugha imechunguzwa kwa kirefu na Palmer (1996)¹ na kuonyeshwa kuwa huwa haihusu neno au makundi ya maneno tu, bali pia miundo ya sentensi na tungo maalumu (kama vile methali, nahau, na nyinginezo).

Katika sehemu hii tutaonyesha tu makundi ya maneno yanayoonyesha kufungana na mazingira ya kiutamaduni na hivyo kutokuwa na visawe katika lugha nyingine. (Mifano ya tungo nyingine itajidhihirisha katika sehemu zinazofuata). Tazama mifano ifuatayo ya makundi ya maneno yanayoeleza maana kuu fulani na tafsiri tunazozitolea. Hii inadhihirisha kuwa lugha zinatofautiana katika mgawanyo wa vivuli vya maana kuu na hivyo kuwa na viwakilishi ambavyo wakati mwingine havipatikani katika lugha nyingine:

¹ Palmer (1996: 113) huita dhana hii “world views”, yaani mitazamo ya dunia ambayo anasema ndio huongoza lugha na namna nyingine za kujieleza kama vile michoro, miziki, uchongaji, na kadhalika Hii kwa kifupi ni kwamba mazingira mahsusi ya binadamu huathiri namna zao mbalimbali za kujieleza.

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

(5) <u>Kiingereza</u>	<u>Kiswahili</u>
(a) <i>two</i> = mbili	(a) <i>juzi</i> = <i>the day before yesterday</i>
(b) <i>twofold</i> = mara mbili	(b) <i>jana</i> = <i>yesterday</i>
(c) <i>double</i> = maradufu	(c) <i>leo</i> = <i>today</i>
(d) <i>twice</i> = mara mbili	(d) <i>kesho</i> = <i>tomorrow</i>
(e) <i>second</i> = -a pili	(e) <i>kesho kutwa</i> = <i>the day after tomorrow</i>
(f) <i>dual</i> = -a uwili	(f) <i>mtondo</i> = <i>3rd day after today</i>
(g) <i>pair</i> = jozi	(g) <i>mtondogoo</i> = <i>4th day after today</i>

Mifano katika (5), inadhihirisha nafasi ya maneno na hasa pale yanapobainisha vivuli tofauti-tofauti vya maana kuu moja. Hapa lugha huweza kutofautiana katika ubainisho na hivyo kufanya dhana mahsusi kwa lugha moja kukosa kisawe chake au kuwa ngumu kutafsiri katika lugha nyingine. Tafsiri ya maneno ya Kiingereza kwa Kiswahili inaonyesha Kiswahili hakina ubainisho mpana wa hii dhana kuu wakati tafsiri ya maneno ya Kiswahili kwa Kiingereza inaonyesha Kiingereza hakina visawe vya maneno yaliyowekewa alama ya swali.

Ama suala jingine kuhusu neno au maneno katika tafsiri ni lile la neno kuwa la kawaida, (yaani linalosikika mara kwa mara kutokana na kueleza mambo ya kawaida ya siku hadi siku na hivyo kuzoeleka) au kuwa ‘gumu’, (yaani lisilozoeleka au lenye kueleza dhana dhahania). Tofauti hizi hujitokeza zaidi kuhusiana na mada zinazojadiliwa katika matini zinazofanyiwa tafsiri. Jambo muhimu hapa ni kwamba hata kama mada itatokea kuwa ngumu, kwa maana ya kuhusika na masuala yasiyozoeleka au dhahania, ni vema mfasiri ajaribu awezavyo kutumia maneno ya kawaida au yaliyozoeleka. Hii hurahisisha maelezo na kufanya neno kuhisika kimaana (taz. kwa mfano Ohly 1976: 84)².

Mwisho, katika mjadala wa maneno katika tafsiri, tunaweza pia tukahusisha majina ya pekee (ya watu, viumbe na nchi). Itakumbukwa kwamba katika tafsiri kama ya Biblia (taz. Dammann (1977: 90-91) ilibidi majina mengi ya kigeni yabadilikebadilike kuchukua maumbo yanayoendana na kanuni za lugha ya tafsiri. Lakini hadi sasa hata jina kubwa kama ‘Kristo’ bado linajitokeza pia kama ‘Kristu’ (katika Kiswahili), ‘Kilisiti’ (katika Kinyakyusa), miongoni mwa waumini wanaotumia lugha hizo. Kwa bahati nzuri majina ya nchi tayari yamekwishaandaliwa orodha kwa Kiswahili na hivyo ni vema kwa wafasiri kujipatia orodha kama hiyo kuwasaidia kupata tafsiri sahihi.

3. Tafsiri na miundo sahihi ya sentensi

Kama tulivyokwishadokeza katika (1) hapo juu, kila lugha huwa ina kanuni na taratibu zake za kupanga maneno kuunda sentensi. Mipangilio hii inaweza kukaribiana kwa lugha za jamii moja na ikatofautiana sana baina ya lugha za jamii tofauti. Hii iliwapanya wataalamu waainishe lugha kulingana na mpangilio wa vipashio vyake katika sentensi. Kwa hiyo, kuna lugha zenye mpangilio wa *kiima – kiarifu – yambwa* (kama vile Kiswahili na lugha nyingine

² Hii hujitokeza zaidi kuhusiana na zile mada za kidini (kiroho) au za kifasihi neno linapotarajiwa kuingiza hisia kwa msomaji au msikilizaji.

za Kibantu, Kiingereza, na nyinginezo), *kiarifu – kiima – yambwa* (kwa mfano Kiarabu) na *kiarifu – yambwa – kiima*.

Lakini, japokuwa katika migawanyo hii mikubwa Kiingereza na Kiswahili zinaweza kuainishwa pamoja, lugha hizi hutofautiana kwa namna nyingine nyingi za uundaji wa sentensi zake. Kwa mfano, wakati katika lugha ya Kiingereza Kiima ni lazima kiwe dhahiri kila wakati, katika Kiswahili kipashio hicho kinaweza kuwakilishwa ndani ya Kiarifu kama katika (6):

- (6) (a) *Juma came home / he came home*
(b) (Juma) alirudi nyumbani

(6a) ni mfano wa sentensi ya Kiingereza ambayo ni lazima ibebe Kiima ‘Juma’ au kiwakilishi chake ‘he’ na (6b) ni sentensi ya Kiswahili ambayo si lazima ionyeshe Kiima ‘Juma’. Badala yake uwakilishi wa kiima hicho kwa kiambishi [a] katika kiarifu husadifu kabisa muundo wa sentensi sahihi katika Kiswahili. Lakini katika Kiswahili, kiambishi [a] huwakilisha ‘he’ na ‘she’ katika Kiingereza. Hivyo, katika sentensi ya Kiswahili ambayo Kiima si dhahiri, mfasiri lazima atafute miktadha mingine ya maelezo ili kujua kama mhusika wa tendo ni mwanaume au mwanamke. Hiyo isipofanyika maana inaweza ikavurugika.

Kiswahili na Kiingereza pia hutofautiana katika upangaji wa vipashio vingine katika sentensi. Kwa mfano, wakati katika Kiingereza vivumishi hutangulia nomino, katika Kiswahili vipashio hivyo hufuata nomino kama inavyoonyeshwa katika (7) hapa chini:

- (7) (a) *a good boy* = mvulana mzuri
(b) *three tall tables* = meza tatu ndefu
(c) *two dirty smelling fish* = samaki wawili wachafu wanaonuka

Katika (7), pamoja na hiyo tofauti ya mpangilio wa nomino na vivumishi baina ya Kiswahili na Kiingereza, hudhihirika tofauti nyingine muhimu. Kwa upande wa Kiingereza, tunaona kuwa lugha hii ina kipashio [a] katika (7a) ambacho hakipo katika Kiswahili. Kwa upande wake Kiswahili kinaonyesha kuwa na viambishi vya upatanishi wa kisarufi ambavyo vinaandamana na vivumishi. Viambishi hivyo ndivyo vinavyodhihirisha miundo inayokubalika katika lugha hii. Vipengele kama hivi ni lazima vitiliwe maanani wakati wa tafsiri.

Katika hatua hii tungependa pia tutoe mfano wa mpangilio ambao ni mahsusi kwa Kiingereza na ambao umekuwa ukijitokeza sana katika sentensi za Kiswahili katika vyombo vya habari nchini Tanzania. Huu ni mpangilio katika (8):

- (8) *That god created man is a fact we can't deny* “kwamba mungu alimuumba mtu ni ukweli ambao hatuwezi kuukana” badala ya “mungu kumuumba mtu ni ukweli ambao hatuwezi kuukana”

Katika (8), kipashio ‘that’ kimetangulizwa katika sentensi ya Kiingereza. Katika lugha hiyo, miundo inayotanguliza kipashio hicho inakubalika kisarufi. Lakini katika Kiswahili miundo inayotanguliza kisawe cha ‘that’, yaani ‘kwamba’, haikubaliki kisarufi. Hata hivyo, katika

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

vyombo vya habari nchini Tanzania, sentensi kama hiyo katika (8) huwa zinatafsiriwa kwa kutanguliza neno ‘kwamba’ na kutoa muundo ambao si sahihi kisarufi katika lugha hii.

Suala jingine linalohusu miundo ambalo ni muhimu kisarufi ni lile la kuwepo kwa miundo inayosadifu kwa uwanja fulani tu na si mwingine. Kwa kawaida, huwa kuna miundo ya sentensi inayobainika waziwazi kuwa ni ya uwanja fulani mahsusi. Hivyo kuna miundo ya sentensi inayobainika kuwa ni ya kisheria, ya kisayansi, ya kidini, ya kawaida, na kadhalika. Kwa mfano, sentensi katika uwanja wa sheria huwa ni ndefu na zenye kuhusisha vipengele vingi vya taarifa. Kutokana na hali hiyo sentensi kama hizo huwa ni ngumu kutafsiri. Hebu tujaribu kutafsiri mfano huu katika (9) na kuona kama inawezekana kuzingatia kanuni za kisarufi vilivyo:

- (9) *Subject to the provisions of section 93, every application for maintenance or for custody of children, or for any other matrimonial relief whatsoever shall, unless included in a petition for a declaratory decree or for annulment, separation or divorce, be by summons in the chamber.*

Sentensi hii ya muundo wa kisheria katika (9), sisi tumejaribu kuitafsiri kama ifuatavyo:

Kwa mujibu wa vifungu vya sehemu ya 93, kila ombi la utunzaji au la malezi ya mtoto, au la msaada wowote ule wa kindoa, isipokuwa pale lilipoingizwa ombi la amri ya kutangazwa, au kwa ajili ya kubatilishwa, kutengana au kuachana, litafanywa kwa kuitwa shaurini mahakamani

Hatuna hakika, kwanza, kama tumetafsiri kifungu hicho vizuri na, pili, kama hiyo tafsiri yetu kwa Kiswahili bado ni lugha ya sheria au lugha ya kawaida tu. Haya ndiyo maswali muhimu ya kisarufi ambayo mfasiri hana budi kuyazingatia kila wakati.

Aidha ingefaa tudokeze hapa pia kwamba ugumu tuliouona kuhusiana na muundo katika (9) hauhusu tu lugha ya uwanja mahsusi. Hapa, hata lugha ya kawaida inaweza ikawa tatizo hasa muundo unapohusisha masuala ya utamaduni wa lugha kama ilivyodokezwa katika sehemu iliyotangulia (taz. pia Qorro 2004). Kwa mfano maelezo katika (10) hapa chini ni tafsiri kwa Kiingereza ya hadithi kutoka katika mojawapo ya lugha za wenyeji wa asili wa Amerika wa huko Amerika. Hapa kuna jina la mnyama (‘Coyote’) ambaye ni wa hukohuko na pengine hakuna aina ya mnyama wa kumlinganisha naye huku Uswahilini. Pili hadithi inayoelezwa ni dhahiri si rahisi kubaini maana yake katika mazingira yetu hapa. Hebu tuone mfano huo.

- (10) *Coyote went off. He saw a man throwing up his eyes. He ran and said “My eyes come back again!” Then they dropped into his sockets again. Coyote said “My gr-gr-gr-grandfather knew that trick too. Do you think you are the only one who knows it?” He took out his eyes and threw them up. “Come drop back, my eyes!” But the man ran and caught them and Coyote had no eyes.*” (kutoka Palmer (1996: 115)

Mbweha wa jangwani aliondoka. Alimwona mtu akitupa macho yake juu. Alikimbia na kusema “Macho yangu hebu rudini!” Kisha yakarudi tena kwenye tundu la jicho. Mbweha wa jangwani akasema “Ba- ba- ba babu yangu aliujuua ujanja huo pia. Unafikiri ni wewe peke yako ndio ujuao?” Alitoa macho yake na kuyatupa juu. “Rudini tena macho yangu”. Lakini mtu alikimbia na kuyashika na Mbweha wa jangwani hakuwa na macho. (*Tafsiri yangu*)

Ingawa lugha yenyewe iliyomo humu katika tafsiri ya Kiingereza ni nyepesi, kutafsiri kinachosemwa humu kunaweza kukawa tatizo kutokana na muktadha wa hadithi hii na maana yake huko itokako. Ikitafsiriwa tu hivyo ilivyo, tuseme kwa Kiswahili, bado inaweza ikakosa fahiwa kwa wasemaji wa lugha hiyo. Hapa ni dhahiri tutakuwa tunavuka mipaka ya kisarufi, lakini tunachosema pia ni kwamba sarufi isizingatiwe tu kama sarufi bali iwe na nafasi katika kutoa fahiwa halisi. Hii ina maana kuna hali kama hizi ambazo huhitaji unyumbufu wa muundo wa sentensi ili kudhihirisha fahiwa (taz. tafsiri ya miundo maalumu katika sehemu inayofuata).

4. Tafsiri na tungo maalumu

Katika utangulizi (taz. (1) hapo juu) tulidokeza kuwa tungo maalumu katika lugha ni zile zijulikanazo kwa majina mbalimbali kama methali, nahau, misemo na katika orodha hii tunaweza tukaingiza vitendawili. Kila moja ya tungo hizi ina sarufi yake, yaani namna maalumu ya mpangilio wa vipashio ndani mwake. Kama tulivyodokeza katika (1) hapo juu, maana katika tungo hizi huwa si zile za maneno katika tungo zenyewe na hata kama zinafungamana na maana katika tungo (kwa mfano katika methali ‘Haraka haraka haina baraka’ – ‘*Haste is waste*’) bado maana hizo ni pana kuliko zile zinazoonekana mara moja. Pili, tungo hizi ndizo zimefungamana na misingi ya kiutamaduni hata kuliko maneno na sentensi tulizozijadili katika sehemu zilizotangulia. Hii hufanya kuwe na haja ya kunyumbua miundo yake zaidi ili kuingiza fahiwa zinazofungamana na mitazamo hii ya kiutamaduni.

Imedhihirika kwamba kumekuwa na matatizo makubwa sana katika kutafsiri tungo hizi. Kwa mfano, Mwansoko (2001) katika uchunguzi wa matatizo ya tafsiri katika vyombo vya habari anaonyesha kwamba pamoja na matatizo ya kutafsiri misamiati na tungo za kawaida yapo matatizo pia ya kutafsiri tungo maalumu kama vile misemo, na nyinginezo. Mifano anayoitoa ni kama hii ifuatayo:

- (11) (a) *corruption cancer* “kansa ya rushwa” badala ya “tatizo sugu la rushwa”;
(b) *Central Police Station* “kituo cha Kati” badala ya “Kituo Kikuu cha Polisi”

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

Mifano hii katika (11) ni miseno ya kawaida katika duru za uchumi, siasa na utawala na inatarajiwa itafsiriwe kwa namna inayofanya msemu ueleweke vizuri. Ni dhahiri kwamba tafsiri zilizotolewa kwa kila msemu katika (11) ni tofauti na ile ya mwisho inaeleweka vizuri kuliko ya kwanza.

Ama kuhusu methali, Qorro (2004: 5f.) anajadili matatizo yanayokabili tafsiri ya aina hii ya tungo maalumu. Tatizo kubwa hasa ni ile mitazamo ya dunia iliyodokezwa katika sehemu zilizotangulia. Anatoa mifano kama hii ifuatayo na kuonyesha kuwa kila mmoja una kipengele ambacho Uswahilini mtazamo wake ni tofauti au kinyume:

(12) (a) *Make the hay while the sun shines* (= Andaa nyasi kwa ajili ya mifugo wakati jua lipo)

(b) *Put it away for a rainy day* (= Iweke hadi inyeshapo mvua)

Methali hizi hutoa picha zilizo kinyume kabisa na hali Uswahilini. Kwa mfano, wakati wa ki-angazi Uswahilini ni kweli ndipo nyasi hukauka, lakini wakati huo ndipo pia nyasi huhitajika zaidi kwa mifugo. Hivyo si wakati wa kuweka akiba bali wa kutumia nyasi zozote zilizopo kwa ajili ya mifugo. Vivyo hivyo, wakati kipindi cha mvua huko Ulaya ni wakati wa shida, huku Uswahilini hicho ndicho kipindi cha baraka watu wasipohitaji akiba yoyote, kwani ndio wakati wa kuzalisha, yanapopatikana maji, mboga, na vinginevyo kwa urahisi.

Hebu tufikirie pia kuwa methali zifuatazo za Kiswahili zingepata tafsiri gani katika lugha kama Kiingereza au lugha nyingine:

(13) (a) Hasira ya mkizi furaha ya mvuvi (= *Cuttle-fish's anger is the fisherman's joy*)

(b) Mchumia juani hulua kivulini (= *A plucker in the sun eats in the shade*)

Sarufi ya methali hizi hudokeza kuwa ile katika (13a) imeibuka katika mazingira ya pwani wakati ile katika (13b) imeibuka katika mazingira ya tropiki. Mazingira hayo ni muhimu katika kupata maana ya methali hizi. Hata hivyo, kwa watu wanaoishi nje ya tropiki methali katika (13b) inaweza ikawa na hali kama ile tuliyoiona katika (12). Kwani wakati katika tropiki jua huashiria shida au ugumu, nje ya tropiki jua ni mali adimu inayotafutwa kuwatia watu joto.

Hebu tupate pia mifano michache ya tafsiri za vitendawili. Vitendawili, kwa kawaida, vina miundo sahili na tatizo huwa zaidi fumbo lililomo ndani mwake. Katika mifano ya vitendawili tuliyo nayo inaonekana kuwa tafsiri zake ni sisisi. Kwa mfano, Mbughuni (1983: 13-18) anajadili vitendawili alivyovitafsiri kama inavyoonekana katika (14):

(14) (a) Othman mfupi kapanda basi la bure. = *Little Othman got a free ride on the bus.*

(b) Inzi katua kwenye upara. = *The fly landed on a bald head.*

(c) Ninasafiri bila kufika. = *I travel without arriving.*

(d) Shamba langu hupaliliwa baada ya kuvuna. = *My shamba is weeded after harvest.*

Vitendawili vingi ni vya miundo kama hiyo katika (14). Miundo hiyo ni sahili kwa kiasi kikubwa na ingeweza kutafsiriwa kisisi kama inavyodhihirika katika mifano hiyo. Cha muhimu hapa ni ikiwa tafsiri kama hizo zinaweza pia zikamrahisishia, tuseme msemaji wa lugha ya Kiingereza, namna ya kufumbua fumbo, yaani kubaini kuwa (14a) ni ‘nzi’, (14b) ni ‘ndege’ (eroplani), (14c) ni “nchi isiyokuwa na ndugu” na (14d) ‘upara’. Na hapa, na pengine tofauti na methali, unaweza kukuta kuwa unyumbuaaji wa muundo wa tafsiri hausaidii katika kupata kupata fahiwa inayoweza kusaidia kufumbua fumbo.

Tungependa tumalizie sehenu hii kwa kurejea kwenye makusanyo ya methali za Kikuria yaliyofanywa na E. Chacha (1999). Katika makusanyo haya Chacha hutoa tafsiri ya Kiswahili na ya Kiingereza ya kila methali na kisha fasiri yake. Kama inavyodhihirika katika (15) hapa chini, tafsiri iliyofanywa ni sisisi. Cha muhimu kuchunguza ni kama zinaweza kueleweka bila fasiri ya methali iliyofanywa:

- (15) (a) *Amanche tegagutira inguku.* “Maji hayapandi mlima.” “*Water never flows up the mountain.*” (*Problems happen where there is weakness.*)
- (b) *Amogooro tegana amaiso.* “Miguu haina macho.”; “*Feet have no eyes.*” (*Feet cannot stop one from going into danger.*)
- (c) *Egete kenokeraaguturi niga ogiichabeta.* “Ukiona kijiti kinaelekea jichoni mwako kipishe.” “*When you see that a stick is pointing to your eye, move away from it.*” (*You have to run away from any kind of evil / serious danger for your safety.*)

Katika (15), tafsiri za Kiswahili na Kiingereza za methali hizi ni sisisi, yaani ya neno kwa neno. Lakini ni dhahiri kwamba katika hali hiyo fahiwa ya methali haijitokezi vizuri kama inavyoonekana katika maelezo ya Kiingereza katika mabano. Maelezo haya kwenye mabano humsaidia msemaji wa Kiingereza kupata fahiwa ya methali kwa kuwa zimenyumbua muundo ili kudhihirisha fahiwa. Lakini miundo yenyewe katika mabano si ya kimethali. Njia bora zaidi ingekuwa kupata methali katika lugha ya Kiingereza iliyo sawa au yenye kuikaribia hiyo. Kwa wasemaji wa Kiswahili, pamoja na kwamba lugha hizi ni za jamii moja na kwamba miundo inalingana, bado fahiwa zilizomo katika methali hazidhihiriki vizuri. Hapa pia miundo ya Kiswahili japokuwa inalingana na ile ya Kikuria, bado hatuwezi kusema kuwa ni ya kimethali. Inawezekana pia Kiswahili kina methali zake zinazolingana au kukaribiana na hizo na ndizo zingeweza kutumika kama tafsiri.

5. Hitimisho

Katika makala haya tumejadili vipengele vya kisarufi ambavyo ni muhimu kuvizingatia katika tafsiri. Vipengele hivyo ni maneno au istilahi zinazosadifu muktadha wa maelezo na miundo ya sentensi inayofuata kanuni za lugha. Kipengele kingine ni kile kinachohusu kile tulichokiita miundo maalumu, yaani ile iliyofungana na mitazamo ya dunia ya wahusika wa lugha. Tumeona kwamba katika tafsiri kuna fahiwa zinazotakiwa kujitokeza ili maana iweze kudhihirika ilivyo katika lugha chanzi. Ildhihirika kuwa mara nyingi fahiwa huwa hazijitokezi waziwazi tafsiri inapokuwa sisisi. Kwa hiyo, wakati mwingine inabidi muundo katika tafsiri unyumbuliwe ili uweze kudhihirisha hizo fahiwa.

UZINGATIFU WA SARUFI KATIKA TAFSIRI

Ama kuhusu miundo maalumu, njia nzuri kabisa ya kuitafsiri ni kuitaftia visawe vyake katika tafsiri. Ikibidi itafsiriwe tu basi ni muhimu miundo ya tafsiri inyumbuliwe ili kupata fahiwa za mitazamo ya dunia iliyokitwa katika tamaduni na mazingira ya lugha husika.

Marejeo

- Chacha, E. P. 1999. *Collection of 104 Kuria proverbs*. Muswada ambao haujachapishwa. Musoma: Maryknoll Language School.
- Dammann, E. 1977. Some problems of translation of the Bible into African Languages. *Kiswahili* 47,2: 88-95.
- Idarous, A. 1995. Tafsiri katika Vyombo vya Habari Tanzania. *Kiswahili na Vyombo vya Habari*, imeharirirwa na S. A. K. Mlacha. Dar es Salaam: TUKI. Uk. 54-63.
- Kihore, Y. M. 1990. Linguistics and Translation from and into African Languages. *Problems of Translation in Africa: Proceedings of the Round-Table Conference. FIT – UNESCO. Dar es Salaam 28-30 August 1989*, FIT Newsletter 9/1&2: 47-52. [Dar es Salaam: FIT].
- Makunja, G. S. 1995. Sarufi na Msamiati wa Kiswahili katika Vyombo vya Habari, *Kiswahili na Vyombo vya Habari*, imeharirirwa na S. A. K. Mlacha. Dar es Salaam: TUKI. Uk. 14-24.
- Massamba, D. P. B., Y. M. Kihore & Y. P. Msanjila. 2004. *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbughuni, P. 1983. Riddles, food for thought. Katika: *Kiswahili* 50,1: 13-18.
- Mugambi, P. J. 2001. Language Conflict in Literacy Translation: Imbuga's 'Betrayal in the City' ('Usaliti Mjini'), *Kiswahili: A Tool for Development. The Multidisciplinary Approach*, imehaririwa na N. I. Shitemi, M. M. Noordin, A. I. Opijah & D. M. Mukuria. Nairobi: Moi University Press. Uk. 225-230.
- Mwansoko, H. J. 1996. *Kitangulizi cha Tafsiri*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mwansoko, H. J. 2001. *Matatizo ya Tafsiri katika Vyombo vya Habari*. Muswada ambao haujachapishwa, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Mwansoko, H. J. 2004. *Umuhimu wa Istilahi katika kufanikisha tafsiri*. Muswada ambao haujachapishwa, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Nasution, S. 1988. Methods, Art and Style of Translation, *International Federation of Translators (FIT) Newsletter* N, VIII.

YARED M. KIHORE

- Ohly, R. 1976. Mapitio: The translation of the Bible into African Languages, *Kiswahili* 46,1: 82-84.
- Palmer, C. B. 1996. *Towards a Theory of Cultural Linguistics*. Austin: University of Texas Press.
- Qorro, M. 2004. *Uzingatiaji wa Utamaduni wa Watumiaji wa Lugha kama nyenzo ya kufanikisha tafsiri*. Muswada ambao haujachapishwa, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.